**LBE KOMPUTA NA INTANETI KIPINDI CHA 3**

Mwandishi : Richard Lough

Muhariri: Katrin Ogunsade

Tafsiri: Eric Ponda

**Wahusika:** Beatrice (Msichana wa makamu), John (Mvulana wa makamu), Sauti yaInternet , Mtaalam ( sauti ya mwanamume kutoka Studioni)
**Kutiwa sauti (Kiswahili ):** Mark Sewe (Mvualana wa miaka 19 katika mkahawa wa Intaneti), Elizabeth Maina (Mwanamke katika mkahawa Intaneti)
Msimulizi: Sauti kutoka Studio.

**Music – [Full up for 0:10 then fade under Intro]**

**Intro:**
Hujambo na karibu tena katika mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu Komputa na Intaneti. Katika kipindi hiki tutajifunza kuhusu huduma za mtandao wa Intaneti na jinsi mtandao huu unavyofanya kazi.

**Package 3.1**

**SFX_Muziki: unaombatana na masuala ya Kisayansi**

**1. Intaneti** : John, Beatrice, Karibuni kwa mtandao wa Intaneti.!.

**2. John:** Nilikuwa nikidhani kuwa mtandao wa Intaneti ni kama anga.Sikuweza kuelewa ukubwa wako.

**3.Intaneti** : Ni kweli. Ningekuwa na mwili, ningekuwa nikinunua nguo mpya kila siku kwasababu nakua kwa haraka kila siku!!

**Fade out SFX_ Muziki uinaoambatana na masuala ya Kisayansi**

**4.Beatrice**: Sasa wewe ni nani au labda nisema ni nini?

**5. Intaneti** : Kwanza kabisa nielewe mimi kama mfumo unatumiwa kuunganisha na kupeperusha huduma za mawasiliano kwa njia ya komputa kote ulimwenguni.

**6. John**: Wewe ndiye mtandao wa Ulimwengu ?

**SFX_Buzzer [as you would hear on a game show for ‘wrong answer’]**

**7. Intaneti** : Hapana.. hapana. Hayo ndio makosa tunayofanya. Mimi na mtandao wa Ulimwengu ni mambo mawili tofauti kabisa.

**8. Beatrice**: Sasa ndio nimetatizika zaidi kuliko tulivyoanza mazungumzo yetu..

**SFX_Sci_Fi_ Sauti ya Komputa**

| | |
|---|---|
| **9. Intaneti**: | Hebu nikueleze. Kama nilivyotangulia kusema mimi ni mfumo tu unaotumiwa kuunganisha huduma za Komputa. |
| **10. John**: | Lakini unaziunganisha vipi huduma hizi, kwa kutumia nyaya? |
| **11. Intaneti**: | Hasa,! hivyo ndivyo nilivyoanza kuhudumu, lakini kadri teknolojia inavyozidi kupanuka na kuimarika,mahitaji au matumizi ya nyaya hizi yataanza kupotea. Siku hizi tunatumia pia ***Satellite..*** |
| **12. Beatrice**: | Sasa mtandao wa Ulimwengu ni nini? |
| **13. Intaneti** : | Mtandao huu kama ninavyoujua, ni mkusanyiko wa hati na rasilimali zinazounganishwa pamoja. |
| **14. John**: | Kwa hivyo Mtandao huu wa Ulimwengu unapatikana kwa ule wa Intaneti? |
| **15. Intaneti**: | Hapana John. Mtandao huu ni miongoni mwa huduma ninazotoa. Kuna huduma nyingine pia kama vile Barua pepe au ***Emails*** . Umewahi kusikia kuhusu ***Emails….***? |
| **16. Beatrice**: | Kama vile ***hotmail*** na ***yahoo-mail***… |

**17.Intaneti**: Hasa!.

**18. John**: Kwa hivyo mtandao huu unaukubwa gani? Tunaweza kujua ni hati ngapi , picha, Muziki, kanda za Video na kadhalika, vinavyohifadhiwa kwenye mtandao huu.?

**Fade in SFX_Sci_Fi_Music_2**

**19. Intaneti**: Kwa kweli hakuna Mtu ajuaye ni kiwango gani au mambo mangapi yanayoweza kuhifadhiwa katika mtandao huu. Lakini yanaweza kufika mabilioni na mabilioni…….

**20. John**: Ni maajabu… na ni vipi unaweza kutumia mtandao huu?

**21. Intaneti**: Mambo yote yanayohifadhiwa kwenye mtandao, yameunganishwa kwa kutumia huduma zijulikanazo kama ***hyperlinks***…

**22. John/Beatrice**: ***Hyperlinks??***

**23. Intaneti** : Hizi ni programu zenye anuani zinazoiwezesha Komputa yako kutafuta habari kutoka kwa komputa nyingine zinazohifadhi habari hizi.

**SFX_** **Akitafuta mtandao kwenye komputa, kwa mfano** www.dw-world.de, mtandao wa Deutsche Welle.

**24. John**: Kwa hivyo kwanza tunahitaji nini kufungua huduma hizi?

**25. Intaneti**: Kwanza kabisa unahitaji Data au Programu kukujiunganisha na nami .

**26. Beatrice**: Programu hiyo ndio inayofahamika kama mtandao wa ugunduzi yaani ***Internet Explorer*** au ***Firefox?***

**27. Intaneti**: Ndio . Mtandao huu wa ugunduzi ndio unaoweza kukuunganisha na huduma zote na kumwezesha mtumiaji kutoka huma moja hadi nyingine kupitia ule mfumo wa huduma za kiunganishio yaani ***hyperlinks*** tuliozungumzia hapo awali.

**28. Beatrice**: Na ni wapi utaweza kupata wapi huduma hizi?

**29. Intaneti**: Iwapo Komputa yako haina huduma hizi, unaweza kuziweka wewe mwenyewe. Lakini Mtu anahitaji kuunganishwa na kampuni au shirika liinalotoa huduma za Intaneti yaani ***Internet Service Provider*** au kwa kifupi ***ISP,*** ambapo mara nyingi huwa ni kampuni ya simu au shirika la mawasiliano.

**30. Beatrice**: Tumezo huduma hizi za ***ISP*** kwenye komputa yetu, Komputa yetu imeunganishwa . Kwa hivyo tunaweza kuanza kukutumia?

**31. Intaneti**: Ndio munaweza !

**32. John**: Lakini iwapo kuna kurasa za tovuti nyingi tu kwenye mtandao huu, utajiunganisha vipi na ule unaotafuta?

**33. Intaneti** : Ikiwa hujui ukurasa wa tovuti unaotafuta, naweza kuupata kupitia huduma za utafiti yaani ***'search engine'.*** Kwa mfano ***Google*** na ***Yahoo.*** Kurasa za tovuti hizi hukusaidia kutafuta unachokitaka kwenye mtandao kwa kuandika neno au jina lenyewe.

**34. Beatrice**: Kwa hivyo unamaana unapoandika jina au neno, mara moja unapata unachokitafuta?

**35. Intaneti**: Ndio. Hebu jaribu. Tuko katika mtandao wa **www.google.com.** Unataka kutafuta nini ?

**36. John**: Ehh…. Bayern Munich?

**37. Intaneti**: Sawa…Andika neno hilo…

**SFX_Akiandika Bayern_Munich**

**38. Intaneti**: Bonyeza ***search*** yaani kutafuta kwenye kibao chako cha Komputa…

**SFX_Akibonyeza mara moja**

**39. Intaneti** : Subiri… sasa tumepata. Mtandao huu wa ***Google*** umepata zaidi ya kurasa milioni 26 zinazohusiana na … kwanza kabisa ni mtandao wa klabu yenyewe .

**40. John**: Maajabu !

**Muziki – Full up for 0:10 then fade under Intro_3.2**

**SFX_Ambie_EasySurf**

**Clip: 3.2_Sewe_EasySurf_ 1**

Naitwa Mark Sewe. Nina umri wa miaka 19. Tuko katika mkahawa wa EasySurf unatoa huduma za Intaneti katika mtaa wa in YaYa centre jijini Nairobi Kenya.

**1.Beatrice**: Mark ni mteja wa mara kwa mara katika mkahawa huu wa EasySurf . Nilimuliza kwanini atumie huduma za Intaneti kila siku?

**SFX_EasySurf_akiandika kwenye komputa**

**Clip: 3.2_Sewe_EasySurf_2**

Kakangu anaishi nchini Ukraine. Na kila mara mimi hutaka kuwasiliana naye. Unajua Ukraine ni nchi ya baridi, na ndio maana hutaka kuwasiliana naye kila wakati ili kumpa motisha. Pia hupenda sana kuwandikia marafiki zangu na isitoshe, kuna huduma za mawasiliano ya moja kwa moja kupitia Mtandao huu wa Intaneti. Kwa hiyo huduma hizi zinaweza kukuunganisha na marafiki,kukupa habari muhimu au kupata data unazohitaji…

**2. Beatrice**: Jiji la Nairobi ni moja wapo ya miji iliyostawi miongoni mwa mataifa yaliyoko kusini kwa jangwa la Sahara. Jiji hili lin idadi ya watu wasiopungua milioni tatu hivi. Lakini hata katika miji mingi mikubwa barani Africa sio mikahawa yote inayotoa huduma za Intaneti ambazo ni bora na za Teknolojia ya haraka. Hivyo basi kwa Mtu kama Mark ni lazima apate mkahawa wenye huduma bora na za haraka zenye kuaminika.

**Clip: 3.2_Sewe_EasySurf_3**

Mimi hupenda mkahawa huuu kwasababu una Komputa za kisasa na zinazotoa huduma za haraka ambazo Mtu anaweza kupata habari atakazo kwa haraka zaidi. Nyingi ya mikahawa haina komputa nzuri, zimechakaa na kufunguka pole pole sana.

**3.Beatrice**: Ukitazama, sio tu Mark anayependa mkahawa huu. Mkahawa wenyewe unajula ya Komputa 20 ambazo zote zinatumika kwa sasa. Wateja pia huleta ***Laptops*** zao. Sio mikahawa yote inayoweza kukuunganisha kwa haraka. Na hapa Mark anatahadharisha dhidi ya mikahawa ya aina hii.. …

**Clip: Sewe_EasySurf_4**

Ni jambo la kuvunja moyo sana. Unaweza kutumia pesa nyingi na muda wako kutafuta habari au kurasa moja tu. Katika mikahawa hii kunalipishwa kwa kila dakika inayotumia komputa.

**4. Beatrice**: Kwa hivyo kasi ya komputa ni muhimu ili kukuondolea dhiki unapotumia mtandao. Usione haya kuwauliza wenye mikahawa hii kuhusu kasi ya kuunganisha huduma hizo kabla ya kuanza kuzitumia. Kuna mikahawa mingi inayotoa huduma hizi jijini Nairobi , lakini najiuliza kwanini mkahawa huu wa EasySurf umeibuka maarufu zaidi kuliko mikahawa mingine. Elizabeth Maina, ambaye huwaelekeza wateja anasema kuwa miongoni mwa huduma bora zaidi wanazotoa ni zile za kuwasiliana moja kwa moja yaani ***Chat Programmes***.

**Clip: 3.2_Maina_Easysurf_2**

Huduma hizi unaweza kutumia ukurasa wa tovuti ya ***messenger,au skype***. Mara nyingi hu wahimiza wateja watumie ***Laptop*** zao, lakini pia unaweza kutumia komputa zetu ambazo pia zina kasi. Wakati huo huo ukitaka kutumia mtandao wa ***Yahoo messenger,*** unaweza kuzungumza, na wakati huo huo kusoma au kuandika barua zako kwa wakati mmoja. Kwa raia wa Uchina wanatumia ule wa ***QQ…***

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**5. Mtaalam** : Hebu sasa Beatrice,nikueleze nini maana ya ***Skype*** . Ni programu inayokuwezesha kupiga simu kwa kutumia mtandoa wa Intaneti. Ili kuweza kutumia huduma hizi unahitaji simu na kipaza sauti.

**X-fade into SFX_Ambie_EasySurf_1 + SFX_Easysurf_Typing**

**9. Beatrice**: Nadhani vifaa tunavyohitaji ni vile vya aina ya Webcam, spika,kwani mara nyingi utakuta mkahawa ambao hauna vifaa hivi na hutaweza kupata unachotafuta hata kama huduma hizo zinaweza kukuunganisha.

Huyo alikuwa mtaalam wetu na tunakushukuru kwa maelezo yako. Hata hivyo Mark bado ana maswali kuhusu ubora wa mkahawa wa kutoa huduma za Intaneti. …

**Clip: 3.2_Sewe_EasySurf_6**

**Outro**

Ni hayo tu kwa leo ambapo tumejifunza yale unayopasa kujua unapotafuta mikahawa wa huduma za Intaneti . Pia Tumejifunza kwamba mkahawa mzuri ni ule unaoweza kukuunganisha kwa haraka, wenye komputa nzuri na kwa gharama nafuu..Mikahawa yote mizuri ni lazima iwe na mtambo wa kuchapisha na Mdaki yaani ***Scanner,*** ingawa utalipishwa zaidi kwa huduma hizi. Na pia mikahawa mizuri ni lazima iwe na vifaa kama vile spika za kutumia wakati wa mawasiliano ya moja kwa moja. Je ungependa kujua jinsi Beatrice na John watakavyogundua ulimwengu wa barua pepe yaani ***Emails?*** Ungana nasi wiki kwa kipindi kijacho au unaweza kutembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe.
Hadi wakati mwengine kwaheri!